

WAHUSIKA WAKUU NI NANI?

Idara ya Utafiti, Takwimu, Upimaji na Ramani ya Kenya

Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo, Kenya

Shirika la huduma kwa Wanyamapori la Kenya

Taasisi ya Utafiti wa Maliasili ya Norway, Norway

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, Norway

Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Tanzania

Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, Tanzania

Chuo Kikuu cha Copenhagen, Denmark

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania

Chuo Kikuu cha Glasgow, Scotland, Uingereza

Chuo Kikuu cha Groningen, Uholanzi

Chuo Kikuu cha Hohenheim, Ujerumani


Taasisi ya uhifadhi ya Ujerumani



This project has received funding from the European Union's Horizon 2020 research and innovation programme under grant agreement

HUDUMA ZA MFUMO IKOLOJIA

Wanadamu hupata kiasi kikubwa cha mahitaji muhimu kutoka Mifumo ikolojia ya asili na bioanuwai zilizomo ndani yake. Huduma za mifumo ya ikolojia hujumuisha faida za moja kwa moja kama vile chakula kutokana na kilimo au uvuvi, maji, motisha na ustawi wa maisha bora, mapato kutokana na shughuli za utalii na faida zisizo za moja kwa moja kama vile kuzuia mafuriko na magonjwa, n.k



MAWASILIANO

AfricanBioServices inaratibiwa na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Norway, Trondheim, Norway.

Barua pepe: <http://africanbioservices.eu>



‘Huduma za mfumo ikolojia ni muhimu kwa ustawi wa maisha Jamii?’




AfricanBioServices

WAPI?

Mfumo ikolojia wa Serengeti-Mara, Tanzania na Kenya



Mabadiliko Tabia nchi



Mabadiliko tabia nchi ni tishio kubwa kwa bioanuai ya dunia na mfumo ikolojia wa Serengeti-Mara tayari mabadiliko haya yameanza kuonekana hususani ongezeko la mabadiliko na kutotabirika kwa mvua.


NINI?

AfricanBioServices ni mradi wa utafiti unaofadhiliwa na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU) unaochunguza Ufanyaji kazi, na huduma za mfumo ikolojia wa Serengeti-Mara (Tanzania na Kenya) na kuathirika kwa mfumo huu kutokana na shughuli za binadamu na mabadiliko tabia nchi.

KWANINI?


Kusudi kuu la mradi wa utafiti ni kupata ufahamu wa kwa namna gani mabadiliko tabia nchi yanayoendelea, ongezeko la idadi ya watu, na mabadiliko ya matumizi ya ardhi yanavyo athiri bioanuai (viumbe hai) na maisha ya ustawi wa jamii, na kutumia taarifa hizi kupata mapendekezo ya mkakati maalum wa kurekebisha athari hizo kwa maendeleo endelevu.

Ongezeko la idadi ya watu



Bara la Afrika linaongoza kwa ukuaji haraka wa idadi ya watu duniani, ambayo inaendana na uhitaji mkubwa wa maliasili, hivyo uhitaji ndani ya Mfumo ikolojia wa Serengeti-Mara unaongezeka

Mabadiliko ya matumizi yaardhi



Maendeleo ya kilimo na viwanda yanabadili matumizi ya maeneo mbalimbali, na kwenye Mfumo ikolojia wa Serengeti-Mara mazingira ya asili yanabadilika kwa haraka

